

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb.Na.IMC/FB.2911/F.7

Tarehe: 11/8/2022

VICHWA BRANDS (T) CORPORATION LTD.  
S.L.P  
DAR – ES – SALAAM.

**Yah: MAOMBI YA UTHIBITISHO WA ENEO LA KIWANDA KIDOGO (SERVICE  
TRADE ) KWAAJILI YA KUUNGANISHIA PIKIPIKI ZA MAGURUDUMU  
MATATU (BAJAJ).**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji inakili kupokea barua yako isiyokuwa na kumbukumbu namba ya tarehe 6/8/2022 ukiomba kupata barua ya uthibitisho ili upate Leseni ya kuendesha shughuli tajwa hapo juu Mtaa wa Mazizini Kata ya Ukonga.

3.Baada ya kukagua eneo lako, Ofisi imebaini kuwa eneo unalomba ni tengefu kwa matumizi ya makazi na makazi na biashara, aidha kwakuwa shughuli yako ni ya kibiashara, utaruhusiwa kuendesha kiwanda kidogo cha kuunganisha pikipiki za matairi matatu (Bajaj) kwa angalizo kuwa, hutoruhusiwa kutumia vifaa au mitambo yenye kusababisha bugdha kama vile kelele, moshi, au aina nyingine yeyote yenye kuleta kero au kuchafua mazingira kwa kipindi chote cha uendeshaji wa biashara yako.

4. Iwapo itabainika kuwa umekiuka masharti hayo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yako ikiwemo kufungiwa kiwanda chako bila taarifa nyingine.

5.Kwabarua hii, Ofisi inashauri apewe Leseni.

Nakutakia kazi njema

**Kny: Mkurugenzi wa Jiji**

**Nakala:** Msajili wa Kampuni na Biashara(BRELA) - (kwa taarifa).